

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



“Mtaa wa Bagara  
Miyomboni,  
S.L.P. 386,  
27103 MANYARA,  
Barua Pepe: [rbcmanyara@pccb.go.tz](mailto:rbcmanyara@pccb.go.tz).  
**TANZANIA.**  
[www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

**MANYARA – NOVEMBA 16, 2020**

**HAKIMU MFAWIDHI AHUKUMIWA MIAKA MITATU**

Hakimu wa Mahakama ya Wilaya Babati Mheshimiwa I. B. KUPPA amemhukumu kwenda jela miaka mitatu au kulipa fine ya shilingi milioni moja na laki tano (Sh.1,500,000/=) aliyekuwa Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Mwanzo ya Magugu **ADELTUS RICHARD RWEYENDERA**

Rweyendera amepewa adhabu hiyo katika kesi ya rushwa namba CC. 137/2020 baada ya kupatikana na hatia kwa makosa ya kuomba na kupokea rushwa ya shilingi 150,000/= kinyume na k/f cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na rushwa na 11/2007

Rweyendera aliomba fedha hizo toka kwa wazazi na ndugu wa washitakiwa wanne ambao walikuwa wanashtakiwa kwenye kesi namba 242/2020 ikiwa ni kishawishi cha kuwasaidia na kuwaachia washitakiwa hao kwenye kesi tajwa ambayo hakimu huyo alikuwa anaisikiliza katika Mahakama ya Mwanzo Magugu.

Hukumu hiyo ilitolewa 13/11/2020 na Mheshimiwa I. B. KUPPA baada ya waendesha mashtaka wa TAKUKURU Martin Makani na Evelyne Onditi kuwasilisha ushahidi Usioacha shaka dhidi ya mshtakiwa Rweyendera kwa mujibu wa sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai 1985 hivyo Mahakama ikamkuta na hatia na kutoa adhabu kwa mujibu wa sheria

Awali TAKUKURU Mkoa wa Manyara ilipokea taarifa kutoka kwa wasiri ikifafanua kuwa Hakimu aliomba kiasi hicho cha fedha akiwataka wazazi na ndugu wa washtakiwa hao wachangishane.

Baada ya kupokea taarifa hiyo ofisi yetu ilifanya uchunguzi wa kina na kubaini kuwa ni kweli kesi tajwa ilikuwepo katika mahakama ya mwanzo Magugu na kwamba kesi hiyo ilikuwa inasikilizwa na hakimu **ADELTUS RICHARD RWEYENDERA**.

Uchunguzi wetu pia ulibaini kuwa wananchi hao walikamatwa kwa tuhuma za uzururaji miongoni mwao wakiwa kwenye maeneo yao ya biashara. Uchunguzi ulibaini kuwa kwa kuwa washitakiwa walikuwa watatu, hakimu aliwataka wachange elfu hamsini kila mmoja na kufanya jumla ya shilingi laki moja na elfu hamsini.

Baada ya kujiridhisha na ukweli huo maafisa wetu waliandaa mtego wa rushwa na kufanikiwa kumkamata hakimu akiwa amepokea kiasi hicho cha shilingi 150,000/= fedha ambazo aliziweka kwenye droo ya meza yake mara baada ya kuzipokea. Rweyendera alifikishwa Mahakama ya Wilaya Babati tarehe 20/08/2020 akapatikana na hatia na kuhukumiwa tarehe 13/11/2020.

Ni Rai yetu kwa wananchi kama alivyosema Mheshimiwa Dr. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hotuba yake ya uzinduzi wa Bunge tarehe 13/11/2020 kwamba, wara rushwa bado wapo kwenye utumishi wa umma hivyo wananchi waendeleo kutoa taaarifa ili tuendeleo kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria

**Imetolewa na**

HOLLE MAKUNGU  
MKUU WA TAKUKURU (M)  
MANYARA